JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2022

## URAIA NA MAADILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2022

# 06 URAIA NA MAADILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI ..... 3
2.1. Swali la 1. Kuwa Mwajibikaji ..... 3
2.2. Swali la 2. Kuheshimu Jamii ..... 11
2.3. Swali la 3: Kuwa Mstahimilivu ..... 17
2.4. Swali la 4: Kuithamini Jamii ..... 24
2.5. Swali la 5: Kuwa Mwadilifu ..... 29
2.6. Swali la 6: Kudumisha Amani ..... 37
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ..... 44
4.0 HITIMISHO ..... 45
5.0 MAPENDEKEZO ..... 46
*Kiambatisho* ..... 47

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2022 katika somo la Uraia na Maadili. Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji katika somo hili.

Ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu wa SFNA 2022 ni mzuri kwani wanafunzi 1,350,477 (84.85%) walifaulu. Aidha, wanafunzi 241,135 (15.15%) hawakufaulu. Taarifa imebainisha kuwa wanafunzi waliofaulu walielewa matakwa ya maswali na walikuwa na uelewa wa kutosha katika mahiri mbalimbali zilizopimwa. Wanafunzi walioshindwa walikuwa na uelewa mdogo wa mahiri zilizopimwa, kushindwa kubaini matakwa ya maswali, kushindwa kuhawilisha maarifa na kukosa ujuzi wa kujibu baadhi ya maswali kama vile; ufahamu, kuchunguza picha na maswali ya majibu mafupi. Aidha, chati ya ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kwa mwaka 2021 na 2022 imewekwa kuonesha jinsi wanafunzi walivyofaulu katika kila swali (umahiri uliopimwa).

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa taarifa hii itawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuboresha ufaulu katika mitihani ijayo ya upimaji wa kitaifa.

Baraza linapenda kutoa shukrani za dhati kwa maafisa mitihani na wengine wote walioshiriki katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili ulifanyika tarehe 27 Oktoba 2022. Jumla ya wanafunzi 1,718,896 walisajiliwa kufanya upimaji huu ambapo wanafunzi 1,591,989 sawa na asilimia 92.62 walifanya upimaji huu. Aidha, ufaulu wa wanafunzi katika somo hili unaonesha kuwa wanafunzi 1,350,477 sawa na asilimia 84.85 walifaulu na wanafunzi 241,155 sawa na asilimia 15.15 hawakufaulu. Ufaulu huu umeshuka kwa asilimia 6.35 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo wanafunzi 1,423,379 (91.20%) walifaulu upimaji ilihali wanafunzi 137,439 (8.8%) hawakufaulu. Hata hivyo, takwimu hizi zinaonesha kuwepo kwa ongezeko la usajili wa wanafunzi 37,127 (2.16%) na 31,171 (1.96%) waliofanya upimaji.

Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Darasa la Nne somo la Uraia na Maadili mwaka 2022 ulikuwa na jumla ya maswali sita (6) yaliyogawanyika katika sehemu A na B yakiwa na vipengele 25. Sehemu A ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele 13 vyenye jumla ya alama 26. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) yenye vipengele 12 vyenye jumla ya alama 24. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu A na B. Upimaji ulikuwa na jumla ya alama 50. Katika sehemu A, swali la kwanza lilikuwa na vipengele vitano (I – V) vya kuchagua jibu sahihi ambapo wanafunzi walitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku. Swali la pili lilikuwa na vipengele vinne vya kuoanisha na liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu majukumu ya viongozi wa wanafunzi katika Kifungu A na vyeo vyao katika Kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Swali la tatu na la mwisho katika sehemu hii lilikuwa la kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi. Kila kipengele cha swali katika sehemu hii kilikuwa na uzito wa alama 2, hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 26.

Aidha, katika sehemu B, swali la nne lilikuwa na vipengele vinne ambapo wanafunzi walitakiwa kujibu kwa kuonesha matendo ya

utunzaji wa mazingira au matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku. Katika swali la tano, wanafunzi walipewa picha ambayo walitakiwa kuichunguza na kisha kujibu maswali manne (4) waliyopewa. Swali la mwisho katika sehemu hii ni swali la sita (6) ambalo liliwataka wanafunzi kusoma kifungu cha habari kwa umakini na kisha kuandika majibu katika sehemu zilizoachwa wazi.

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji wa somo la Uraia na Maadili imejikita katika kuchambua maswali yote sita yaliyotoka katika mahiri sita kama zilivyoainishwa katika muhtasari wa somo la Uraia na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III - VII. Uchambuzi huu pia unabainisha idadi au asilimia ya wanafunzi walioweza au walioshindwa kuchagua majibu sahihi na sababu zilizowafanya wachague majibu hayo.

Viwango vya ufaulu wa jumla vimegawanywa katika makundi matatu ya ubora wa ufaulu kwa kuzingatia asilimia ya wanafunzi waliofaulu katika swali husika. Lengo la kufanya hivyo ni kurahisisha na kujenga uelewa wa haraka kuhusu ufaulu wa wanafunzi. Hivyo, kiwango cha ufaulu cha asilimia 0 – 33 ya wanafunzi katika swali kinahesabika kuwa ni hafifu, 34 – 66 ni wastani na asilimia 67-100 ni kiwango kizuri. Viwango hivi vya ufaulu wa jumla vimewakilishwa na rangi tofauti: nyekundu (ufaulu hafifu), njano (ufaulu wa wastani) na kijani (ufaulu mzuri) katika jedwali la uchambuzi wa ufaulu (ona kiambatisho). Hivyo, ulinganifu wa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika kila umahiri na maswali katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2021 na 2022 ni kama unavyoonekana katika kiambatisho.

Mwisho, katika uchambuzi wa kila swali viwango vya ufaulu wa wanafunzi vimewekwa katika makundi manne ambayo ni ufaulu mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu. Pia, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa wanafunzi katika swali husika, ambapo rangi ya kijani, kijani kibichi, njano na nyekundu zinawakilisha kiwango cha ufaulu mzuri sana, mzuri, wastani na hafifu mtawalia.


## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inachambua ufaulu wa wanafunzi katika kila swali (umahiri) kwa kuonesha jumla ya wanafunzi waliofanya swali husika na kuelezea ubora wa majibu yao. Pia, viwango vya ufaulu wa wanafunzi katika kila swali vimewekwa katika makundi manne ambayo ni ufaulu mzuri sana, mzuri, wastani na dhaifu. Lengo ni kuonesha kiwango cha utendaji cha wanafunzi katika swali husika kwa kuzingatia mgawanyo wa alama katika swali hilo.

### 2.1. Swali la 1. Kuwa Mwajibikaji

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa Kuwa Mwajibikaji. Swali lilikuwa la kuchagua herufi ya jibu sahihi na lilikuwa na vipengele vitano (i) – (v) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 2. Aidha, kila shina la swali katika kila kipengele lilikuwa na machaguo manne (A – D) ambapo mwanafunzi alitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika katika kisanduku katika karatasi ya mtihani. Kwa ujumla, maswali katika vipengele vitano yalipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa dhana mbalimbali zinazohusiana na kuwa mwajibikaji na namna zinavyotumika katika maisha yake ya kila siku.

Takwimu zinaonesha kuwa swali hili limejibiwa vizuri zaidi na wanafunzi ikilinganishwa na maswali mengine. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 1,086,524 (68.25%) kati ya 1,591,989 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama 4 hadi 10. Aidha, wanafunzi 505,465 (31.75%) walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 hadi 2. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1




**Chati Na. 1***: Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 1 umefanyika kama ifuatavyo:

(i) Mtu anayetekeleza majukumu yake ipasavyo anajulikana kama
  A msikivu.
  B mtiifu.
  C mwaminifu.
  D muwajibikaji.

Kipengele hiki cha swali kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia majukumu yanayomhusu mwanafunzi nyumbani na shuleni* na lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua sifa anayopewa mtu anayetekeleza majukumu yake ipasavyo. Wanafunzi walioweza kubaini jibu sahihi, D *Mwajibikaji,* walikuwa na uelewa kuwa mwajibikaji ni mtu anayetekeleza majukumu yake ipasavyo; hujitoa kikamilifu katika kutekeleza wajibu wake kwa kufanya kile anachotakiwa kukifanya. Mwajibikaji hupanga mambo yake na kutoa maamuzi sahihi kabla ya kutekeleza. Huweza kujisimamia na kuonesha nidhamu ambayo inawafanya wengine kumwamini. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kwamba kama wanafunzi, wana wajibu wa kuwasaidia wazazi wao katika shughuli mbalimbali za nyumbani kama vile; kuwalea wadogo zao, kufua nguo, kufanya

usafi wa mazingira ya nyumbani. Pia wana wajibu wa kutekeleza majukumu ya shuleni ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu walimu na wazazi wao.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua kipotoshi B, *Mtiifu*. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha na hivyo kushindwa kubaini kuwa mtu mtiifu ni yule ambaye yupo tayari kutekeleza agizo lolote kutoka kwenye mamlaka halali kama atakavyoelekezwa. Wanafunzi walipaswa kuelewa kuwa mtu anaweza kuwa mtiifu kwasababu tu sheria na taratibu zinamtaka kufanya hivyo, lakini mwajibikaji hutekeleza majukumu yake bila kulazimishwa na sheria au kanuni zilizopo. Kwasababu hiyo, mtu anaweza kuwa mtiifu lakini asiwe mwajibikaji.

Vilevile, kipotoshi C, *Mwaminifu* na A, *Msikivu* hayakuwa majibu sahihi. Kwa mfano, wanafunzi waliochagua kipotoshi C hawakujua kuwa mwaminifu ni mtu anayeaminika kuwa mwema na mkweli, hawezi kumdhuru au kumdanganya mtu mwingine. Hata hivyo, hali ya kuwa mwema au mkweli haimpi mtu uhalali wa kuwa anatekeleza majukumu yake ipasavyo bali sifa ya uwajibikaji hutegemea namna mhusika anavyojitolea kutekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa. Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi ulibaini kuwa wanafunzi wengine walichagua kipotoshi, A *msikivu* kwa kutokuelewa kuwa msikivu ni sifa ya mtu ambaye akionywa husikia na kuzingatia yale anayoelezwa. Hivyo, wanafunzi hawa walishindwa kutambua kuwa sifa ya kuwa msikivu haina mahusisano ya moja kwa moja na mtu anayetekeleza majukumu yake ipasavyo. Swali la pili lilikuwa kama ifuatavyo:

(ii) Lipi ni mojawapo ya majukumu ya mtoto katika familia?
- A Kuheshimiwa na familia
- B Kupendwa na familia
- C Kusikilizwa na familia
- D Kujali mali za familia

Kipengele hiki cha swali kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kusimamia Majukumu ya Nyumbani na Shuleni* na ulilenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini majukumu ya mtoto katika familia.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi D, *Kujali mali za familia* walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na kusimamia majukumu ya nyumbani na shuleni na hivyo kuweza kuchagua jibu sahihi*.* Wanafunzi hawa walikuwa na ufahamu kuwa mtoto kama sehemu ya familia ana majukumu ya kufanya ikiwa ni pamoja na kulinda rasilimali na mali za familia kama vile vyombo, majengo na samani. Pia, walifahamu kuwa, majukumu mengine ya mtoto katika familia ni kuwasaidia wazazi kuwalea wadogo zao, kushiriki katika shughuli za maendeleo ya familia, kusaidia kuwahudumia ndugu wa familia hasa nyakati ngumu kama kuugua au matatizo mengine mbalimbali. Vilevile, majukumu ya kufanya usafi wa mazingira ya nyumbani, kulisha mifugo, kufua na kuosha vyombo.

Aidha, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi; A, *Kuheshimiwa na Familia,* B, *Kupendwa na Familia* na C, *Kusikilizwa na Familia.* Machaguo yote haya hayakuwa majibu sahihi kwasababu yanahusiana na haki na wajibu wa mtoto au mzazi/mlezi katika familia. Kwa mfano, Kipotoshi A, *Kuheshimiwa na familia* ni miongoni mwa haki ya mtoto katika familia inayomuonesha kuwa yeye ni wa thamani na niwa muhimu katika familia yake. Hivyo, wanafunzi hawa walishindwa kutambua kuwa kitendo hiki humsadia mtoto kujijengea hisia kuwa anaaminika na pia yupo salama. Vilevile, kipotoshi B, *Kupendwa na Familia* siyo jibu sahihi kwakuwa kupendwa na wazazi au walezi ni haki mojawapo ya mtoto katika familia. Wanafunzi hawa hawakutambua kuwa kumuonesha upendo mtoto ni muhimu kwa maendeleo ya afya ya akili na ukuaji kwa ujumla.

Kwa upande wa wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Kusikilizwa na Familia* hawakuwa na uelewa kwamba watoto wana haki ya kusikilizwa na wanaweza kushiriki katika maamuzi ya familia yanayoweza kuwaathiri kulingana na umri wao. Kwahiyo, watoto wana uhuru wa kutoa maoni yao na wazazi/walezi wanawajibika kuyaheshimu na kuyazingatia. Pia, ni vema kuelewa kuwa haki nyingine za watoto zitapatikana endapo wazazi watatimiza majukumu yao mengine kama vile: kuwalinda watoto dhidi ya hatari, kuwapatia watoto elimu, huduma ya afya na mahitaji ya lazima kama vile chakula, mavazi na malazi.

(iii) Vitendo vifuatavyo vinaonesha jinsi watu wanavyothamini rasilimali zetu, **isipokuwa**
- A kupanda miti.
- B kulinda wanyamapori.
- C kuchoma misitu.
- D kutunza vyanzo vya maji.

Kipengele hiki cha swali kilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *Kulinda Rasilimali na Maslahi ya nchi* ambapo lilipima uwezo wa mwanafunzi kuelewa wajibu wake wa kulinda rasilimali na maslahi ya nchi. Swali liliwataka wanafunzi kubaini kitendo ambacho si cha kuthamini rasilimali zetu miongoni mwa vitendo vinavyoonesha jinsi watu wanavyothamini rasilimali zetu vilivyoorodheshwa kwenye machaguo A – D.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi C, *kuchoma misitu* walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu rasilimali zetu na namna ya kuzitunza kama vile wanyama pori, maji, udongo, mafuta, misitu, gesi na vito vya thamani kama madini. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kuchoma misitu ni kitendo cha makusudi au uzembe wa mtu kutupa mabaki ya moto au sigara kwenye msitu na kupelekea kuwasha moto. Pia, walielewa kuwa moto usiopangiliwa na kudhibitiwa kwenye misitu unachukuliwa kuwa ni uharibifu wa mazingira kwasababu unadhoofisha ubora wa hewa na wakati mwingine kusababisha vifo vya watu na wanyama, uharibifu wa mali na mazao. Vilevile, kuchoma misitu kunasababisha ardhi kuwa wazi na hivyo kusababisha mmomonyoko wa udongo kutokana na upepo au mvua na kusababisha hali ya jangwa. Pia, inaonesha kuwa wanafunzi hawa walielewa umuhimu wa kutunza na kuthamini mazingira kama vile kutunza misitu kwa sababu inatoa makazi ya wanyama, kuzuia mafuriko na inasaidia michakato ya asili ya kimazingira kufanya kazi vizuri kama vile utengenezaji wa udongo. Misitu pia hutoa mandhari nzuri kwa ajili ya kupumzika na kustarehe.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi; A, *Kupanda miti*, B, *Kulinda Wanyamapori* na D, *Kutunza Vyanzo*

*vya Maji* ambayo hayakuwa majibu sahihi. Wanafunzi hawa walishindwa kubaini kuwa majibu yote haya ni matendo ya kuthamini rasilimali zetu. Kwa mfano, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kupanda Miti*, hawakuwa na uelewa wa kutosha kuwa upandaji miti husaidia kuhifadhi mazingira kwa kusafisha hewa kwa kufyonza hewa ya kabonidayosaidi na kuchuja maji tunayokunywa. Vilevile, miti inasaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo na ni makazi asilia na chakula kwa viumbe mbalimbali.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *kulinda wanyamapori* hawakuelewa kuwa ni jitihada za kuhakikisha ulinzi kwa wanyamapori kwa kudhibiti, kupunguza au kuondoa uharibifu unaofanywa na binadamu kwa wanyamapori. Juhudi hizi ni pamoja na kuanzishwa kwa hifadhi na mbuga maalum kwa ajili ya wanyamapori ambazo zinalindwa kwa sheria mahususi ili kuhakikisha zinaendelea. Baadhi ya mbuga hizo ni Mikumi, Ngorongoro, Ruaha na Serengeti.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Kutunza Vyanzo vya Maji*, hawakuwa na uelewa kwamba maji ni rasilimali muhimu kwa uhai wa viumbe duniani hivyo, inapaswa kulindwa. Hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kutunza rasilimali hii muhimu ikiwemo kupanda miti karibu na vyanzo vya maji, kupiga marufuku shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji, kukataza umwagaji na utiririshaji wa vitu hatarishi kwenye vyanzo vya maji. Hatua nyingine ni kutunga sheria za kulinda vyanzo vya maji kwa mfano, sheria ya usimamizi wa vyanzo vya maji Na.11 ya mwaka 2009 na kuanzishwa kwa mamlaka za uhifadhi wa mabonde ya mito kama vile wa bonde la mto Wami.

(iv) Watu wanaotembea pembeni mwa barabara hujulikana kama

A Madereva
B Polisi wa Trafiki
C Waenda kwa miguu
D Wamachinga

Kipengele cha nne cha swali hili kilitoka katika umahiri mahususi wa *Kutii Sheria na Kanuni katika Kutekeleza Majukumu ya Kila*

*Siku*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua sheria za usalama barabarani. Katika swali hili wanafunzi walitakiwa kuchagua neno/jina ambalo linatambulisha watu wanaotembea kwa miguu pembeni mwa barabara. Jibu sahihi ni C, *Waenda kwa Miguu.* Jibu hili lilichaguliwa na wanafunzi ambao walitambua kuwa waenda kwa miguu ni watu wanaotembea kwa miguu pembeni mwa barabara. Wanafunzi hawa walitambua kuwa watembea kwa miguu kama watumiaji wengine wa barabara, wanatakiwa kuhakikisha wanafuata kanuni zote za usalama barabarani kwa usalama wao.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha kati ya watembea kwa miguu na madereva, hivyo wakachagua kipotoshi A, *Madereva*. Wanafunzi hao hawakutambua kuwa madereva wanatembea barabarani wakiwa wanaendesha vyombo vya moto kama vile magari madogo, malori, mitambo na pikipiki. Wanafunzi wengine walichagua kipotoshi B, *Polisi wa Trafiki*. Kundi hili la wanafunzi lilishindwa kutambua kuwa polisi wa trafiki au askari wa usalama barabarani ni miongoni mwa kitengo ndani ya jeshi la usalama wa raia chenye jukumu la kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni za usalama barabarani kwa watumia barabara. Katika kutekeleza wajibu wao, askari wa usalama barabarani hutumia njia mbalimbali kama vile kufanya doria kando kando ya barabara na kuanzisha vituo vya muda au vya kudumu kwa ajili ya ukaguzi na kuhakikisha sheria za usalama barabarani zinafuatwa.

Katika mwelekeo huo, wanafunzi waliochagua kipotoshi D, *Wamachinga* walishindwa kutambua kuwa wamachinga hutembea kando kando ya barabara wakiuza bidhaa na kutoa huduma kwenye maeneo ya wazi bila kuwa na majengo ya kudumu kwa ajili ya kufanyia biashara au kutolea huduma. Pamoja na kwamba wamachinga hutembea kwa miguu mitaani kutafuta wateja, wengine hutumia vyombo vya usafiri kama vile gari, pikipiki, baiskeli na mikokoteni katika shughuli zao.

(v) Ni shughuli ipi ya kujitolea kati ya hizi mtoto anaweza kuifanya katika jamii?
   A Kuchimba na kujenga barabara
   B Kuotesha na kutunza miti
   C Kuchimba na kuuza madini
   D Kununua na kuuza maji


Kipengele hiki kilitungwa kutoka kwenye umahiri mahususi wa *Kulinda Rasilimali na Maslahi ya Nchi*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini shughuli za uwajibikaji ambazo mtoto anaweza kujitolea kufanya katika jamii. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi B, *kuotesha na kutunza miti*, walikuwa na uelewa kuwa shughuli za kujitolea ni shughuli ambazo watu hufanya kwa hiari bila malipo yoyote. Wanafunzi hawa walifahamu kuwa mwanafunzi kama sehemu ya jamii anawajibika kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii. Hii inahusisha kushiriki katika shughuli kama vile: kazi za uhifadhi wa mazingira na kulinda Amani, kufanya usafi katika vituo mbalimbali vya jamii, hususani nyakati za mwisho wa wiki, kusaidia kuelimisha jamii kuhusu mambo muhimu kama vile umuhimu wa kuwa na jamii isiyo na migogoro na kushiriki katika kupanda na kuhifadhi miti shughuli ambazo zinaweza kufanyika nyumbani au shuleni.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua kipotoshi A, *Kuchimba na Kujenga Barabara,* walishindwa kuelewa kuwa kazi hizo hujumuisha michakato ya kitaalam na kitaaluma kama vile: kupanga, kuandaa vifaa na rasilimali watu, kufumua ardhi na kudhibiti ubora wa kazi. Hivyo, hizi siyo shughuli ambazo mtoto anapaswa kuzifanya kwani ni hatarishi kwa maendeleo ya kiakili na kimwili kwa mtoto.

Mwisho kabisa, wanafunzi waliochagua vipotoshi C, *Kuchimba na Kuuza Madini* na D, *Kununua na Kuuza Maji* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuwa vipotoshi hivyo viliashiria kitendo cha kufanya biashara. Kwahiyo, kuchimba na kuuza madini pamoja na kununua na kuuza maji hutafsiriwa kama utumikishaji wa watoto. Vitendo hivyo humnyima mtoto kufaidi utoto wake, kipaji chake na utu wake kwahiyo, ni hatari kwa maendeleo ya mtoto kiakili na kimwili

### 2.2. Swali la 2. Kuheshimu Jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* hususani katika umahiri mahususi wa *Kuipenda na Kujivunia Shule Yake*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi juu ya muundo wa uongozi wa shule; hususani uwezo wa wanafunzi kutambua majukumu ya viranja wa shule kwa kuzingatia nafasi zao za uongozi katika serikali ya wanafunzi. Swali liliwataka wanafunzi kuoanisha maelezo kuhusu majukumu ya viongozi wa wanafunzi katika kifungu A na vyeo vyao katika kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: asilimia 38.32 walipata ufaulu wa alama 0 hadi 2, asilimia 22.79 walipata alama 4, asilimia16.19 walipata 6 na asilimia 22.70 walipata alama zote 8. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu wa wastani kwakuwa wanafunzi 981,947 (61.68%) walifaulu kwa kuweza kupata kati ya alama 4 hadi 8 wakati wanafunzi 610,042 (38.32%) walifeli kwa kupata alama 0 hadi 2. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 2 ni kama ifuatavyo:

Swali lilitaka mwanafunzi ajibu vipengele (i) – (iv) kwa kuoanisha majukumu ya viongozi wa wanafunzi katika Kifungu A na vyeo vyao katika Kifungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| **Fungu A** | | **Herufi** | **Fungu B** |
|---|---|---|---|
| (i) | Mwanafunzi anayefuatilia ufundishaji na ujifunzaji shuleni | (   ) | A. Kiranja wa Michezo<br>B. Kiranja wa Miradi<br>C. Kiranja Mkuu<br>D. Kiranja wa Nidhamu<br>E. Kiranja waTaaluma<br>F. Kiranja wa Usafi |
| (ii) | Mwanafunzi anayesimamia majukumu yote ya viranja shuleni | (   ) | |
| (iii) | Mwanafunzi anayehakikisha wanafunzi wanaingia darasani na kuwa na tabia njema | (   ) | |
| (iv) | Mwanafunzi anayehakikisha kuwa shule inavutia na kupendeza muda wote | (   ) | |

Katika kipengele cha (i), swali lilimtaka mwanafunzi kuoanisha cheo cha kiranja wa shule kutoka fungu B kinachoendana na maelezo katika kundi A ya mwanafunzi anayefuatilia mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Wanafunzi ambao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya viranja wa shule waliweza kuchagua jibu sahihi E, *Kiranja wa Taaluma*. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa kiranja wa Taaluma anawajibu wa kusimamia maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wote shuleni. Pia, kiranja wa taaluma anajukumu la kushauriana na uongozi wa shule katika kusimamia maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni kwa lengo la kuboresha ufaulu wa wanafunzi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi A, *Kiranja wa Michezo* walipaswa kuelewa kuwa kiranja wa michezo ana jukumu la kufuatilia shughuli za michezo zinazofanyika shuleni kama vile kupanga matukio ya michezo ya ndani au nje ya shule. Pia, anawajibu wa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanashiriki

katika shughuli za michezo shuleni. Vilevile, anawajibika kutunza vifaa vya michezo vya shule na kushauriana na uongozi wa shule katika mambo yanayohusu michezo. Kadhalika, wanafunzi waliochagua kipotoshi B, *Kiranja wa Miradi* walishindwa kuelewa kuwa kiranja wa miradi hawajibiki na ufuatiliaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji katika shule; badala yake anawajibika kusimamia shughuli zote za kujitegemea ikiwa ni pamoja na kupanda mbogamboga katika shamba au bustani ya shule. Pia, hushauri uongozi wa shule kuanzisha miradi mbalimbali inayoweza kuiingizia shule mapato.

Vilevile, wanafunzi waliochagua kipotoshi C, *Kiranja Mkuu*, hawakuelewa kuwa Kiranja Mkuu ni kiongozi mkuu wa serikali ya wanafunzi na msimamizi mkuu wa viranja wote shuleni. Yeye ni kiongozi wa baraza la wanafunzi, ni kiunganishi kati ya wanafunzi na walimu au mwakilishi wa wenzake/shule katika matukio/shughuli mbalimbali za wanafunzi nje ya shule. Pia, Kiranja Mkuu huwa ni mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wengine.

Wanafunzi wengine walikosea kwasababu walioanisha na kipotoshi D, *Kiranja wa Nidhamu*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba Kiranja wa Nidhamu ana jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za shule kwa wanafunzi. Kwa mfano, kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anafika shuleni mapema, anavaa sare ya shule na anakuwa na nidhamu nzuri. Vivyo hivyo, wanafunzi wengine waliooanisha na kipotoshi F, *Kiranja wa Usafi* hawakuwa na uelewa kwamba Kiranja wa Usafi ana jukumu la kusimamia usafi wa mazingira ya shule nzima ikiwemo vyoo na maeneo ya ndani na nje ya madarasa. Pia, anawajibu wa kuhakikisha mazingira ya shule yako safi na yanavutia wakati wote.

Swali la (ii) liliwataka wanafunzi kubaini cheo cha kiranja wa shule kutoka kifungu B kinachoendana na maelezo katika kifungu A kuwa ni mwanafunzi anayesimamia majukumu yote ya viranja shuleni. Baadhi ya wanafunzi waliweza kuoanishana jibu sahihi C, *Kiranja Mkuu.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa Kiranja Mkuu aweza kuwa Kaka au Dada Mkuu wa shule ambaye ni kiongozi na msimamizi mkuu wa wanafunzi wote na shughuli zingine za viranja shuleni.

Pia, Kiranja Mkuu anachaguliwa na wanafunzi wenzake kutumikia nafasi hiyo kwa muda maalum uliopangwa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walioanisha na kipotoshi A, *Kiranja wa Michezo* kimakosa. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kwamba Kiranja wa Michezo ni msimamizi wa shughuli zote zinazohusiana na michezo shuleni. Anakuwa na wajibu wa kuandaa timu ya shule katika michezo mbalimbali kama vile: mpira wa miguu, mpira wa wavu, mpira wa pete, mpira wa kikapu na mpira wa mikono. Pia, ana wajibu wa kushirikiana na mwalimu wa michezo kualika timu za shule nyingine kucheza na timu ya shule yake. Zaidi ya hayo, wanafunzi wengine waliooanisha na kipotoshi B, *Kiranja wa Miradi* walikosea kwa sababu wanapaswa kuelewa kuwa Kiranja wa Miradi anawajibika kusimamia shughuli za elimu ya kujitegemea shuleni. Kwa mfano, katika baadhi ya shule Kiranja huyu husimamia shughuli zote za shamba la shule, kulisha mifugo na duka la shule. Vivyo hivyo, wanafunzi waliooanisha kipengele hiki na kipotoshi D, *Kiranja wa Nidhamu* walishindwa kufahamu kuwa Kiranja wa Nidhamu siyo msimamizi mkuu wa miradi ya shule bali ana wajibu wa kudumisha nidhamu ya shule miongoni mwa wanafunzi kwa kuhakikisha kila mwanafunzi anafuata sheria na kanuni zote za shule.

Vilevile, wanafunzi wengine walivutiwa na kipotoshi E, *Kiranja wa Taaluma* kwa kutokujua kuwa jukumu kuu la kiranja wa taaluma ni kuhakikisha na kudumisha ubora wa shule katika taaluma. Kiranja huyu hushirikiana na walimu kutatua changamoto zinazowarudisha nyuma wanafunzi na kusababisha wasifanye vyema kitaaluma. Mwisho, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na jibu lisilo sahihi F, *Kiranja wa Usafi* hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya Kiranja wa Usafi shuleni. Wanafunzi hawa wanapaswa kufahamu kuwa jukumu la Kiranja wa Usafi ni kuhakikisha mazingira ya shule yanakuwa safi na ya kuvutia kila wakati. Pia, kiranja huyu ana wajibu wa kushirikiana na viongozi wengine kuwasimamia wanafunzi katika kufanya usafi wa mazingira ya shule na madarasa.

Swali la (iii) liliwataka wanafunzi kubaini cheo cha kiranja wa shule kutoka kifungu B kinachooana na maelezo kwamba ni mwanafunzi

kiongozi ambaye ana jukumu la kuhakikisha kuwa wanafunzi wenzake wanaingia darasani na kuwa na tabia njema. Jibu sahihi ni D, *Kiranja wa Nidhamu*.  Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya viranja wa shule hasa kiranja wa nidhamu. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kiranja wa nidhamu anasimamia kanuni na taratibu zote za shule kwa wanafunzi na anamsaidia mwalimu wa nidhamu kutoa taarifa na ufuatiliaji wa mwenendo wa tabia zisizokubalika miongoni mwa wanafunzi. Yeye ni mfano wa kuigwa kwa wenzake kwa kigezo kwamba bila nidhamu thabiti, heshima ya shule na ufaulu wa wanafunzi kitaaluma vinakuwa mashakani.

Kinyume chake, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi A, *Kiranja wa Michezo* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya kiranja wa michezo. Wanafunzi hawa walipaswa kufahamu kuwa majukumu, ya kiranja wa michezo hayahusiani na swala la wanafunzi kuingia darasani na kuwa na tabia njema. Kimsingi, Kiranja wa Michezo anasimamia ustawi wa shule katika michezo kwa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata fursa sawa ya kushiriki katika shughuli za michezo. Vilevile, hushirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa vifaa vya michezo kama vile: mipira, neti na viwanja vipo shuleni kwa uwiano unaokubalika.

Aidha, wanafunzi waliooanisha kipotoshi B, *Kiranja wa Miradi*, walipaswa kuelewa kuwa mgawanyo wa mamlaka na majukumu katika muundo wa uongozi wa serikali ya wanafunzi unampa majukumu Kiranja wa Miradi kushughulika na mambo yanayohusiana na miradi ya shule. Kiranja huyu anahamasisha wanafunzi kufanya kazi kwenye miradi ya shule ili kujipatia uzoefu pamoja na ujuzi katika shughuli binafsi. Baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi C, *Kiranja Mkuu* walionesha kushindwa kutofautisha kati ya majukumu ya Kiranja Mkuu na yale ya Kiranja wa Nidhamu. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa Kiranja Mkuu ni kiongozi mkuu katika uongozi wa wanafunzi ambaye anasimamia shughuli zote za wanafunzi na viranja akiwemo kiranja wa nidhamu.

Pia, baadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi E, *Kiranja wa Taaluma* ambalo nalo halikuwa jibu sahihi kwa sababu kipotoshi

hicho kinamuhusu kiranja wa taaluma ambaye husimamia shughuli za ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Kiranja huyo huwashauri wanafunzi wenzake kuhusiana na mambo ya kitaaluma na anatoa taarifa kwa walimu ikiwa kuna changamoto inayozuia kufanya vizuri kitaaluma shuleni. Bbaadhi ya wanafunzi waliooanisha na kipotoshi F, *Kiranja wa Usafi.* Wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majukumu ya kiranja wa usafi shuleni kwasababu jukumu lake sio kusimamia utunzaji wa muda na tabia. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa kiranja wa usafi anahusika na usimamizi wa usafi wa mazingira ya shule kama vile: kufagia, kufyeka majani marefu na kusafisha vyoo.

Mwisho, Swali la (iv) liliwaelekeza wanafunzi kuoanisha kutoka kifungu B jina la cheo cha kiranja wa shule anayehakikisha kuwa shule inavutia na kuonekana safi kila wakati. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu ya viranja wa shule, hasa kiranja anayesimamia shughuli zote za usafi shuleni walioanisha na jibu sahihi F, *Kiranja wa Usafi*. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa kiranja wa usafi ana wajibu wa kusimamia shughuli zote za usafi shuleni. Pia, anawajibika kuhakikisha kuwa mazingira ya shule yana muonekano mzuri kwa kuhamasisha wanafunzi kupanda miti katika eneo la shule, kupanda maua kwenye bustani na kufyeka majani marefu katika maeneo yanayoizunguka shule. Vile vile, kiranja wa Usafi hutoa ushauri kwa uongozi wa shule kuhusu kununua vifaa vya usafi kama: fagio, majembe, fyekeo, sabuni na vitakatishi pindi vinapohitajika.


Kinyume chake, baadhi ya wanafunzi walioanisha na chaguo A, *Kiranja wa Michezo* walishindwa kutofautisha majukumu ya kiranja wa usafi na majukumu ya kiranja wa michezo. Hivyo, iliwapasa kuelewa kuwa Kiranja wa Michezo hujihusisha na usimamizi wa shughuli za michezo pamoja na utekelezaji wa ratiba ya michezo shuleni. Zaidi ya hapo, wapo wanafunzi wengine waliooanisha na kipotoshi B, *Kiranja wa Miradi*. Wanafunzi hawa walipaswa kufahamu kuwa kiranja wa miradi anawajibika kuratibu na kusimamia shughuli zote za kujitegemea shuleni ambazo zinalenga kuwawezesha wanafunzi kujitegemea na kuwa wawajibikaji. Vilevile, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi C, *Kiranja Mkuu*

hawakuelewa kwamba Kiranja Mkuu ni kiongozi mkuu wa wanafunzi katika shule. Kiranja huyu huwakilisha muundo mzima wa uongozi wa wanafunzi katika matukio mbalimbali ndani na nje ya shule. Pia, kiranja mkuu ni kiunganishi kati ya wanafunzi na uongozi katika jumuiya ya shule.

Vilevile, wanafunzi waliovutiwa na kipotoshi D, *Kiranja wa Nidhamu* hawakuwa na uelewa kuwa kiranja wa nidhamu hawajibiki kudumisha usafi shuleni bali anawajibika kushughulika na mambo yote yanayohusiana na nidhamu za wanafunzi. Katika kutekeleza jukumu hili, kiranja wa nidhamu anachangia pakubwa katika kujenga na kudumisha hali ya amani shuleni. Kiuhalisia, Kiranja wa nidhamu yupo karibu zaidi na wanafunzi wenzake, kwahiyo anaweza kushughulika na matatizo ya kinidhamu katika ngazi ya chini kabisa. Zaidi ya hayo, wanafunzi waliooanisha na kipotoshi E, *Kiranja wa Taaluma* walishindwa kuelewa kuwa kiranja wa taaluma anashirikiana na ofisi ya taaluma kusimamia mambo yanayohusiana na ufundishaji na ujifunzaji shuleni. Pia, huushauri uongozi wa shule juu ya mikakati ya kuboresha ufaulu wa wanafunzi kama vile: kufanya mashindano ya midahalo, majaribio ya kushtukiza na kuhimiza wanafunzi kujiunga na vilabu mbalimbali vya masomo.

## 2.3. Swali la 3: Kuwa Mstahimilivu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mstahimilivu.* Wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi lililopo katika mabano na kuliandika kwenye nafasi iliyoachwa wazi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa wastani, kwani wanafunzi 879,901 (55.27%) walifaulu kwa kupata kati ya alama 4 hadi alama 8 ambapo kati yao 313,245 (19.60%) walipata alama 4, 328,949 (20.66%) walipata alama 6 na 237,707 (14.93%) walipata alama zote 8. Hivyo, wanafunzi 712,088 (44.73%) hawakufaulu kwasababu walipata kati ya alama 0 hadi 2. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3.




**Chati Na. 3***: Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 3 ulifanyika kama ifuatavyo:

(i) Kutatua changamoto hutusaidia ______________________
(kufikia malengo yetu, kufanya kazi kwa bidii, kuwa maarufu)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *kuvumilia katika maisha ya kila siku*. Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua faida za kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo katika maisha ya kila siku. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *kufikia malengo yetu*, walitambua kuwa changamoto katika maisha ya mwanadamu ni kitu kisichoepukika na endapo hazitatatuliwa ipasavyo zinaweza kukwamisha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, jambo la msingi unapokumbana na changamoto ni kuwa mstahimilivu, kuikubali na kutafuta namna ya kukabiliana nayo bila kujisababishia matatizo. Baadhi ya changamoto hizo ni kama vile: njaa, matatizo kutoka kwa marafiki na ndugu, kutofanya vizuri masomoni, matatizo ya kiuchumi, msongo wa mawazo, kutotendewa vizuri na matatizo ya kiafya. Vilevile, wanafunzi hawa walifahamu kuwa kufikia malengo ni zao la kufanya kazi kwa juhudi kubwa ili kuyapata matokeo yaliyokusudiwa kwa kuchukua hatua stahiki na mtazamo chanya kukabiliana na changamoto husika.

Mwisho, wanafunzi hawa walitambua kuwa bila kutatua changamoto hatuwezi kuyafikia malengo tuliyojiwekea maishani.

Kinyume chake, wanafunzi waliokosa maarifa ya namna ya kuwa mvumilivu na mstahimilivu katika maisha ya kila siku walishindwa kutambua jibu sahihi kwa kuchagua kipotoshi *kufanya kazi kwa bidii* na *kuwa maarufu.* Kwa mfano, wanafunzi waliochagua *kufanya kazi kwa bidi,* hawakuelewa kuwa kufanya kazi kwa bidii ni kitendo cha kujitoa na kufanya juhudi kubwa kukamilisha jukumu fulani. Kitendo hicho hakiwezi kuwa matokeo ya kutatua changamoto bali ni suluhu ya changamoto zinazosababishwa na uvivu. Kwa kufanya kazi kwa bidii mtu anaweza kupata kipato, kujihisi kuridhika, kufaulu mitihani na kutatua matatizo mbalimbali. Kwa hiyo, mtu huyo anaweza kutatua changamoto ya umasikini, msongo wa mawazo, kutofanikiwa na migogoro ya kifamilia. Vilevile, wanafunzi waliochagua *kuwa maarufu,* walipaswa kuelewa kuwa kupata umaarufu siyo kichocheo cha kutatua changamoto. Hivyo, walishindwa kuelewa kuwa changamoto zinatatuliwa ili kuondokana na vizuizi vya kufikia malengo yetu katika maisha. Zaidi ya hayo, kuwa maarufu kunasababishwa na mambo mengi kama vile kuwa na tabia ya kutaka kupendwa, kuwa na ujuzi wa kuanzisha ushirikiano na mahusiano mazuri, kuwa msaada kwa watu na kuwa na ujuzi wa kuwafanya wengine wajisikie vizuri kuhusu maisha yao. Sababu nyingine inategemea ubora wa mtu kama vile: kuwa mwenye akili na maarifa, mcheshi, mbunifu na kuwa jasiri.

(ii) Mwanafunzi mwenye tabia nzuri ni yule ambaye ____________
(hufanya kazi mwenyewe tu, hushirikiana na wenzake, husaidia walimu tu)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *kujipenda na* kuwapenda wengine na lilipima uwezo wa mwanafunzi kubaini tabia nzuri ambazo mwanafunzi anaweza kuwa nazo. Wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu linaloonesha tabia nzuri ya mwanafunzi kutoka miongoni mwa majibu matatu waliyopewa. Hivyo, jibu sahihi *kushirikiana na wenzake* lilichaguliwa na wanafunzi waliotambua kuwa kushirikiana na wengine ni sifa nzuri inayohusisha kufanya kazi pamoja na watu wengine ili kufikia lengo fulani. Wanafunzi

hawa walifahamu kuwa tabia ya ushirikiano ni uwezo wa mwanafunzi kuweza kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa kuwa kushirikisha na kuthamini mchango wa wenzake. Pia, walifahamu kuwa mwanafunzi anayeshirikiana na wengine huwa na tabia ya kupenda wengine kwa kuheshimu tofauti zao, kutumia lugha ya upole wakati wa kuhitaji kitu, kuwa mtiifu kwa maelekezo kutoka kwenye mamlaka na kugonga mlango kabla ya kuingia mahali popote. Aidha, walitambua pia kuwa kinyume cha kutokuwa na ushirikiano ni kutengwa hali ambayo husababisha kutengwa miongoni mwa watu. Hali hii huambatana na upweke ambao umfanya mtu kujisikia mpweke na kukosa furaha jambo ambalo humfanya mtu kushindwa kufanya kazi ipasavyo ikilinganishwa na watu wenye ushirikiano.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua jibu lisilosahihi *hufanya kazi mwenyewe tu* walipaswa kuelewa kuwa kufanya kazi mwenyewe ni tabia inayoonesha kutoshirikiana na wengine. Mtu wa aina hii hufanya kazi kivyake bila kushirikisha wengine; iwe kazini au shuleni. Vitendo hivi vinafubaza ukuaji wa stadi za kijamii na endapo havitadhibitiwa husababisha matatizo ya kijamii. Madhara ya kufanya kazi bila kuwashirikisha wengine ni kama vile: kutochangamana na jamii, kufanya kazi kupita kiasi, msongo wa mawazo, kukosa taarifa, kutofikia malengo na ufanisi katika kazi, na kukosa faida nyingine za kushirikiana na wenzako. Kitu kibaya zaidi ni kwamba mazoea ya kutoshirikiana na wengine hujenga tabia ya ubinafsi kwa muhusika. Vilevile, baadhi ya wanafunzi waliochagua jibu lisilosahihi *husaidia walimu tu* walipaswa kuelewa kuwa kuwasaidia walimu tu hakuwezi kuashiria mwanafunzi kuwa na tabia nzuri bali inaashiria tabia ya mtu anayefanya vitu kwa uoga. Mwanafunzi mwenye tabia nzuri hatarajiwi kuwasaidia walimu tu, bali anapaswa kumsaidia mtu yoyote mwenye kustahili msaada. Kwa mfano, mwanafunzi mwenye tabia nzuri huwasaidia wazazi kazi za nyumbani, hushirikiana na kuwasaidia wenzake katika kazi za darasani, na huwasaidia wasiojiweza kama wazee na watu wenye ulemavu endapo ikilazimu kufanya hivyo.

(iii) Mawazo mazuri au mabaya aliyonayo mtu juu ya jambo fulani huitwa________________________

(mtazamo, ushirikiano, ustahimilivu)

Swali hili lilitoka katika umahiri mahususi wa *kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu tafsiri ya dhana mtazamo. Wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi ambalo tafsiri yake ni mawazo mazuri au mabaya aliyonayo mtu juu ya jambo Fulani miongoni mwa majibu matatu waliyopewa.

Wanafunzi walioweza kutambua jibu sahihi *mtazamo* walikuwa na uelewa wa kutosha kuwa mtazamo maana yake ni hisia, imani au maoni ya kukubali au kukataa kuhusu kitu, hali au mtu. Pia, walielewa kuwa mtazamo ni majibu ya tahimini ya mtu juu ya kitu au mtu fulani na yaweza kuwa chanya au hasi. Kawaida watu hushauriwa kuwa na mtazamo chanya katika maisha kwa lengo la kuwa na matumaini siku zote kuhusu hali, watu wengine, mahusiano na hata muhusika mwenyewe. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watu wenye mtazamo chanya huwa na tumaini, umakini na huona njia mahali penye ugumu. Kinyume chake, mtazamo hasi husababisha watu kukata tamaa, hivyo hali huwa mbaya zaidi wakati wa hali ngumu. Wanafunzi hawa walitambua umuhimu wa kuwa na mtazamo chanya kwasababu unaweza kuwasaidia kushinda kukata tamaa na hofu kwa urahisi, husaidia kukabiliana na hali kwa kukubaliana nayo, inasaidia kupata funzo kutokana matendo ya watu wengine na kubaki kuwa na mtazamo chanya kuelekea malengo yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, wanafunzi hawa walitambua umuhimu wa kuwa na mtazamo chanya kwa kuwa husaidia kutokata tamaa, kuwa na shukrani, kujifunza na kupokea maarifa kutoka kwa wengine na kuwa makini katika kutimiza malengo yaliyowekwa.

Kinyume chake, wanafunzi waliochagua *Ushirikiano,* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa ushirikiano ni tendo la kufanya kazi na wengine ili kukamilisha jukumu fulani tofauti na mtazamo ambao ni hisia, imani au maoni ya kukubali au kukataa kuhusu kitu au hali, kitu au mtu. Katika maisha ya kila siku katika jamii mbalimbali, watu hushirikiana ili

kufanikisha malengo waliyojiwekea. Hivyo, ushirikiano ni kitu muhimu katika kufikia mafanikio ya kitaalamu au kibinafsi kwasababu unasaidia kufikia malengo, kutatua migogoro, kujenga mahusiano, kuboresha mawasiliano na kupata maarifa mapya.

Vivyo hivyo, wanafunzi waliochagua *ustahimilivu* hawakujua kwamba siyo jibu sahihi na kuwa neno ustahimilivu ni uwezo wa kuwa na subira, mvumilivu na kusonga mbele unapokabiliana na changamoto, matatizo au nyakati ngumu. Pia, ni dhahiri kuwa wanafunzi hawa hawakufahamu kuwa ustahimilivu ni uwezo wa kuvumilia magumu, kuyakubali na kuyakabili kwa mtazamo chanya na kutoteteleka wakati wa shida hizo. Aidha, walipaswa kufahamu kuwa maisha yamejawa na changamoto; kwa hiyo, ili kufikia malengo ya maisha ni lazima kukabiliana na changamoto hizo kwa mawazo chanya huku ikitumainiwa kuwa kuna nafasi nyingine ya kufanikiwa. Ni muhimu pia kujua kuwa sifa binafsi zinazoweza kumsaidia mtu kupambana na kuwa mvumilivu wakati wa shida ni pamoja na kujitambua, kujikubali, kujidhibiti, kuwa na ujuzi wa kutatua matatizo, na uungwaji mkono.

(iv) Watu wa dini tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa amani endapo ________
(watalazimishana kufuata dini moja, watawafukuza watu wasio na dini, wataheshimiana)

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mahususi wa *kuheshimu tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti.* Swali lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua umuhimu wa kuheshimu itikadi na imani za watu tofauti. Wanafunzi walitakiwa kukamilisha sentensi kwa kuchagua jibu sahihi kwenye mabano linaloonesha ni kwa namna gani watu wa dini tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa amani. Wanafunzi waliochagua jibu sahihi *wataheshimiana*, walielewa kuwa kuheshimu dini za watu wengine husaidia kukuza umoja na upendo kati ya watu wa dini tofauti. Hivyo, walitambua kuwa Tanzania ni nchi isiyofungamana na itikadi ya dini yoyote isipokuwa watu wake wana dini; hivyo wananchi wanafurahia uhuru wa kuabudu katika dini walizozichagua. Kuheshimu hilo, wanafunzi wanaruhusiwa kwenda kwenye nyumba

za ibada kuabudu na kushiriki vipindi vya dini shuleni. Zaidi ya hayo, wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa sare za shule kwa kadiri ya imani zao na sikukuu zote za kidini huheshimiwa na dola. Kuheshimu dini au itikadi ya mtu mwingine ni muhimu sana kwa lengo la watu kuishi kwa amani kwani kinyume chake ni kuondoa amani na upendo katika jamii. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika majibu sahihi katika swali la 3.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kutatua changamoto hutusaidia *kufikia malengo yetu*
(kufikia malengo yetu, kufanya kazi kwa bidii, kuwa maarufu)

(ii) Mwanafunzi mwenye tabia nzuri ni yule ambaye
*hushirikiana na wenzake*
(hufanya kazi mwenyewe tu, hushirikiana na wenzake, husaidia walimu tu)

(iii) Mawazo mazuri au mabaya aliyonayo mtu juu ya jambo fulani huitwa
*mtazamo*
(mtazamo, ushirikiano, ustahimilivu)

(iv) Watu wa dini tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa amani endapo
*wataheshimiana*.
(watalazimishana kufuata dini moja, watawafukuza watu wasio na dini, wataheshimiana)

Kielelezo 3.1: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mwanafunzi katika Swali la 3

Kinyume chake, wanafunzi wengine walichagua vipotoshi *watalazimishana kufuata dini moja* na *watawafukuza watu wasio na dini*. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa vipotoshi hivi vinapandikiza chuki na kubaguana miongoni mwa waumini wa dini tofauti hivyo, ni hatarishi kwa uwepo wa amani na uhuru wa kuabudu katika jamii husika. Kwa mfano, kulazimisha watu kufuata dini moja maana yake ni kulazimisha mtu kwenda kinyume na imani yake. Pia ni kinyume na misingi ya nchi yetu ambayo haifungamani na dini yoyote. Matendo ya kulazimisha kufuata dini moja na kuwafukuza watu wasio na dini ni kiashiria cha kutokuwa na uvumilivu wa kidini na ni ukiukwaji wa uhuru wa kuishi utakavyo na kuchangamana. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 3.

3. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuchagua jibu sahihi katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Kutatua changamoto hutusaidia ustahimilivu ________

(kufikia malengo yetu, kufanya kazi kwa bidii, kuwa maarufu)

(ii) Mwanafunzi mwenye tabia nzuri ni yule ambaye

______ kusima ______

(hufanya kazi mwenyewe tu, hushirikiana na wenzake, husaidia walimu tu)

(iii) Mawazo mazuri au mabaya aliyonayo mtu juu ya jambo fulani huitwa

______ Madorefa ______.

(mtazamo, ushirikiano, ustahimilivu)

(iv) Watu wa dini tofauti wanaweza kuishi pamoja kwa amani endapo


______ kufikia malengo ______.

(watalazimishana kufuata dini moja, watawafukuza watu wasio na dini, wataheshimiana)

Kielelezo 3.2: Sampuli ya Majibu ya Mwanafunzi yasiyosahihi katika Swali la 3

## 2.4. Swali la 4: Kuithamini Jamii

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini jamii* na umahiri mahususi wa *kutunza mazingira.* Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini matendo ya utunzaji au uharibifu wa mazingira katika jamii. Swali lilikuwa na vipengele vinne (i) - (iv) na liliwataka wanafunzi kuonesha matendo ya utunzaji wa mazingira au matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: asilimia 43.40 ya wanafunzi walipata 0 hadi alama 2, asilimia 22.16 walipata alama 6, asilimia 18.05 walipata alama 4 na asilimia 16.39 walipata alama 8. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani wanafunzi 901,096 (56.60%) walipata alama kuanzia 4 hadi alama 8 na wanafunzi 690,893 (43.40%) walipata alama 0 hadi alama 2. Chati Na 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4.




**Chati Na. 4**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 4 ulifanyika kama ifuatavyo:

Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuonesha matendo ya utunzaji wa mazingira au matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku.

| Na | Kitendo | Utunzaji wa mazingira | Uharibifu wa mazingira |
|---|---|---|---|
| (i) | Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji. | | |
| (ii) | Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima. | | |
| (iii) | Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng'ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa | | |
| (iv) | Mzee Daudi ameotesha miti mitano kisha anakata mti mmoja kwa ajili ya mbao | | |

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi waliweza kuonesha vipengele vinavyoonesha shughuli za uharibifu wa mazingira. Wanafunzi hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za kutunza mazingira. Pia, walielewa kuwa uharibifu wa mazingira ni vitendo vya kuharibu ubora wa mazingira kwa njia ya kupunguza ubora wa rasilimali kama: hewa, maji na udongo. Wanafunzi walioweka alama ya vema (√) kwenye kisanduku cha kuharibu mazingira katika kipengele (i) *Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji* walifahamu kuwa kutupa taka kwenye mito kunaweza kusababisha maji kutokuwa salama kwa matumizi ya binadamu au wanyama. Walielewa kuwa shughuli nyingine ni umwagaji wa uchafu kwenye bahari, kutiririsha mifereji ya maji machafu kwenye vyanzo vya maji, uvujaji wa mafuta kutoka kwenye vyombo vya majini na kufanya shughuli za kilimo karibu na vyanzo vya maji.

Vivyo hivyo, wanafunzi wengine waliweza kuweka alama ya vema (√) katika kipengele (iii) *Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng'ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa.* kilichoonesha kitendo cha kuharibu mazingira. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa kitendo cha kununua ng'ombe wengi na kuwachunga katika eneo dogo ni uharibifu wa mazingira kwani kitendo hicho kitapelekea mmomonyoko wa udongo kwa njia ya upepo na mvua. Pia, udongo unaweza kupoteza virutubisho na kuathiri uwezo wa mimea kuota. Vyanzo vingine vya uharibifu wa mazingira vinaweza kuwa ni matumizi ya njia mbaya za kilimo, ukataji miti na matumizi makubwa ya mbolea za viwandani.

Uchambuzi zaidi umebainisha kuwa wanafunzi walioweza kuonesha vitendo vya kutunza mazingira na kuweka alama ya vema (√) katika vipengele (ii) na (iv) walikuwa na maarifa ya kutosha kwani walijua kuwa kipengele (ii) *Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima* kilikuwa ni kitendo cha kutunza mazingira. Utunzaji wa mazingira unaweza kudumishwa kwa upandaji upya miti katika maeneo yasiyokuwa na miti au hata kupanda miti mbadala kufidia miti iliyokatwa awali. Wanafunzi walikuwa na uelewa kuwa kitendo cha kumwagilia bustani kwa maji

kutoka kwenye kisima ni shughuli za uhifadhi wa mazingira. Mimea inahitaji maji ili ikue na itengeneze chakula chake kupitia mchakato wa usanisinuru na kupooza. Shughuli nyingine za uhifadhi wa mazingira kama vile: kudhibiti uchafu kutoka viwandani ambayo inachafua hewa na maji, matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, kwa mfano magari ya kutumia umeme na nguvu ya jua. Pia, utupaji mzuri wa taka, matumizi mazuri ya kilimo na uvuvi, kupunguza mifugo, kudhibiti ongezeko la watu na makazi na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi katika swali la 4.

4. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuonesha matendo ya utunzaji wa mazingira au matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku.

| Na | Kitendo | Utunzaji wa Mazingira | Uharibifu wa Mazingira |
|---|---|---|---|
| (i) | Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji. | | √ |
| (ii) | Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima. | √ | |
| (iii) | Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng'ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa. | | √ |
| (iv) | Mzee Daudi ameotesha miti mitano kisha anakata mti mmoja kwa ajili ya mbao. | √ | |

*Kielelezo 4.1: Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4*

Kwa upande mwingine, kulikuwa na wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa yakutosha kuhusu shughuli za utunzaji wa mazingira hivyo walishindwa kuonesha matendo ya utunzaji au uharibifu wa mazingira. Wanafunzi hawa waliweka alama ya vema (√) kwenye kisanduku ilihali ikionesha matendo yasiyo husika. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliweka alama ya vema (√) kwenye kisanduku kuonesha tendo la utunzaji wa mazingira kipengele (i) *Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji*. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa kuhifadhi mazingira kunahusisha shughuli za kudumisha na

kuhifadhi ubora wa mazingira ili kuzuia yasiharibiwe. Kitendo cha kutupa taka mtoni ni uharibifu wa mazingira tofauti na kuyalinda.

Vilevile, kulikuwa na wanafunzi ambao hawakuweza kutofautisha kati ya matendo ya uharibifu na utunzaji wa mazingira na kutunza mazingira, hivyo kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo lisilohusika. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliweka alama ya vema (√) kwenye tendo la uharibifu wa mazingira katika kipengele (ii) *Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima* kitendo ambacho sio sahihi. Wanafunzi hawa walipaswa kuelewa kuwa kumwagilia bustani kwa maji kutoka kwenye kisima ni shughuli za uhifadhi wa mazingira kwasababu mimea inahitaji maji ili ikue na itengeneza chakula chake kupitia mchakato wa usanisinuru.

Aidha, kulikuwa na wanafunzi walioweka alama ya vema (√) kwenye tendo la kuhifadhi mazingira kipengele (iii) *Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng’ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa*. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa kitendo cha kununua ng’ombe wengi na kuwachunga katika eneo dogo ni uharibifu wa mazingira tofauti na kuyatunza. Uharibifu wa mazingira unaoweza kusababishwa na kununua ng’ombe wengi ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, udongo kupoteza rutuba na kuathiri uwezo wa mimea kuota. Kwa ujumla, wanafunzi hawa waliangalia zaidi faida ambayo watoto watapata kwa kupata chai ya maziwa kuliko hasara inayotokana na kuwa na ng’ombe wengi kwa mazingira.

Vilevile, baadhi ya wanafunzi waliweka alama ya vema (√) kwenye kisanduku kuonesha tendo la uharibifu wa mazingira katika kipengele (iv) *Mzee Daudi ameotesha miti mitano kisha anakata mti mmoja kwa ajili ya mbao*. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kutunza mazingira na hivyo kuonesha tendo lisilohusika. Wanafunzi walipaswa kuelewa kuwa kupanda miti mingi kabla ya kukata mti mmoja humaanisha urejelezaji wa miti. Kwa hiyo, kitendo alichokifanya Mzee Daudi kilikuwa na faida katika mazingira kwakuwa upandaji miti huongeza ubora wa udongo, huzuia mmomonyoko wa udongo na huzuia kutokea kwa hali ya

ujagwa. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali 4.

4. Jibu vipengele (i) – (iv) kwa kuonesha matendo ya utunzaji wa mazingira au matendo ya uharibifu wa mazingira kwa kuweka alama ya vema (√) kwenye tendo husika katika kisanduku.


| Na | Kitendo | Utunzaji wa Mazingira | Uharibifu wa Mazingira |
|---|---|---|---|
| (i) | Mwanafunzi anabeba pipa lililojaa taka na kwenda kumwaga mtoni ili zichukuliwe na maji. | ✓ | |
| (ii) | Kumwagilia bustani ya maua kwa kutumia maji ya kisima. | | ✓ |
| (iii) | Eneo la shule ni dogo. Mwalimu mkuu amenunua ng'ombe wengi ili kila mtoto apate chai ya maziwa. | ✓ | |
| (iv) | Mzee Daudi ameotesha miti mitano kisha anakata mti mmoja kwa ajili ya mbao. | | ✓ |

Kielelezo 4.2: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 4*

## 2.5. Swali la 5: Kuwa Mwadilifu


Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwadilifu* na umahiri mahsusi wa *kusimamia haki.* Swali lilipima uwezo wa wanafunzi katika kubaini haki ya mtoto kwa kuangalia picha kwa makini na kisha kujibu maswali katika vipengele vinne (a) - (d).

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: asilimia 68.67 walipata ufaulu wa alama 0 hadi 2, asilimia 19.19 walipata alama 4 wakati asilimia 8.11 walipata alama 6 na asilimia 4.03 walipata alama 8. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kulinganisha na maswali mengine kwani jumla ya wanafunzi 1,093,193 (68.67%) walipata alama kuanzia 0 hadi 2. Wanafunzi wengine 498,796 (31.33%) walipata kuanzia alama 4 hadi alama 8. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 4 ulifanyika kama ifuatavyo:



Maswali

(a) Taja matendo mawili yanayoonekana katika picha.

(i)______________________________________________

(ii)______________________________________________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua matendo yanayoonekana katika picha. Swali liliwataka wanafunzi kutaja matendo mawili yanayoonekana katika picha. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa majibu sahihi yalitajwa na wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kutosha wa kuchunguza picha kwa makini. Vilevile, wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki waliweza kutaja majibu sahihi. Baadhi ya

majibu sahihi yaliyotajwa yalikuwa: *wanafunzi wanakwenda shule* na *mtoto mlemavu anaomba msaada, mtoto anatengeneza kokoto* na *mtoto amesimama mbele ya darasa*. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kwenye picha kulikuwa na mwanafunzi mvulana na msichana wakiwa kwenye sare za shule wakielekea shuleni huku upande wao wa kushoto kulikuwa na mtoto mwenye ulemavu amekaa chini ya mti akiwa amenyanyua mikono mbele kuomba msaada wa fedha kwa wanafunzi waliokuwa wanapita. Upande wa mbele ya picha hiyo, kulikuwa na mwanafunzi aliyesimama mbele ya madarasa na wengine wakitekeleza haki yao ya kupata elimu. Aidha, picha ilionesha msichana aliyekuwa ameshika nyundo mkononi akipasua mawe kutengeneza kokoto. Shughuli ya kuombaomba na kutengeneza kokoto inaonesha ukiukwaji wa haki ya mtoto kupata elimu, kucheza, kupata mlo kamili, kupendwa na kutunzwa na kulindwa. Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwepo kwa wanafunzi waliotaja majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya wanafunzi hawa walishindwa kutafsiri matendo katika picha na wengine walikosa maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotajwa na wanafunzi yalikuwa: *shule* na *mwalimu*, *kitendo kibaya na kitendo kisichoruhusiwa katika jamii, tabia mbaya*, *watoto, kipofu na wanafunzi na mtu anafanya kazi*. Majibu mengine yasiyo sahihi yalikuwa: *mama, utandawazi, watoto kuhusu jamii, kwenda kwenye biashara, mtoto mtiifu* na *haki ya mtoto*.

(b) Ni wajibu gani ambao haujatimizwa na wazazi wa baadhi ya watoto wanaoonekana katika picha? ____________________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini wajibu wa wazazi kwa watoto. Swali liliwataka wanafunzi kutambua wajibu ambao haukutekelezwa na wazazi wa watoto wanaoonekana katika picha. Wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wajibu wa wazazi kwa watoto na ujuzi wa kutosha wa kuchunguza picha kwa makini walitaja majibu sahihi. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotajwa yalikuwa: *wazazi wameshindwa kupeleka watoto shuleni* au *kuwapatia elimu*. Wanafunzi hawa walikuwa na uelewa kuwa ni wajibu wa wazazi kuhakikisha kuwa haki za watoto kama vile: haki ya kupata elimu, kucheza na kupumzika, huduma ya afya,

kupata mlo kamili na kulindwa dhidi ya hatari zinasimamiwa. Haki za mtoto zikikiukwa matokeo yake yanaweza kuwa utumikishwaji wa mtoto, kutokujua kusoma na kuandika, ndoa za lazima au utotoni, kudhuriwa mwili na kushirikishwa katika shughuli za kihalifu. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi ambao walitaja majibu yasiyo sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotajwa yalikuwa: *mvulana yule anakopa wanafunzi wamsaidie, hakuna baba au mama* na *imani ya mtoto kufanya kazi wakati wengine wanaenda shule.* Majibu mengine yasiyo sahihi yalikuwa kama ifuatavyo: *haki ya mtoto, fedha, mtoto anaomba chakula* na *mguu umevunjika*.

(c) Mara unapoona haki za watoto zinakiukwa unatakiwa kufanya nini? ________________________________________


Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutambua hatua za kuchukua wanapoona haki za mtoto zinakiukwa. Swali liliwataka wanafunzi kueleza mambo ya kufanya ili kukabiliana na ukiukwaji wa haki za watoto. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki za watoto waliweza kutoa majibu sahihi. Baadhi ya majibu sahihi ya wanafunzi yalikuwa: *kutoa taarifa, kutoa taarifa polisi, kutoa taarifa kwa Afisa elimu, kutoa elimu kwa wakiukwaji, kuchukua hatua kuzuia na kuwaambia wazazi*. Wanafunzi hawa walielewa wajibu wa wanajamii kuchukua hatua stahiki katika kuzuia ukiukwaji wa haki za mtoto kwa kuweka wazi ukiukwaji huo kwa mamlaka zinazohusika. Walionesha pia, kuzifahamu mamlaka zinazoshughulikia ulinzi wa haki za mtoto kama vile: dawati la jinsia na watoto katika jeshi la polisi na ofisi za Maendeleo ya Jamii.

Kwa upande mwingine, uchambuzi umebaini uwepo wa wanafunzi ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki za watoto. Pia kulikuwa na wanafunzi ambao walikuwa na uwezo mdogo wa kutafsiri picha na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yalikuwa: *nitamsaidia kwa pesa kama ningekuwa nayo, wape chakula, msaidie kupata pesa, nitakwenda kumwambia samahani kwa hilo, saidia mtoto furaha,*

*kupata mlo kamili na pesa.* Wanafunzi hawa wanapaswa kufahamu kuwa ukiukwaji wa haki za mtoto hauwezi kukoma kwa kuwafariji kwa njia ya pesa, maneno, na kitu kingine bali kwa kuchukua hatua madhubuti ili kukomesha ukatili huu. Wanafunzi wengine walieleza *waambie wazazi wake, unapaswa kuwaambia wazazi wake kuwa watoto wana haki ya kupata elimu, ninakwenda kuwa na haki ya kulindwa, lazima umpleke shule, mtoto haki, inaonesha watoto kuhusu familia, katika wingi sherehe, a school, wanakwenda shule, kwasababu ni mtoto wa mtaani, kutumia maskini, kufanya kazi vizuri* na *wengine wanakwenda shule.*

(d) Kwanini kitendo kinachoonekana katika picha ya mtoto mwenye nyundo mkononi ni cha ukiukwaji wa haki za watoto?
____________________________________________
____________________________________________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kuchambua matendo ya ukiukwaji wa haki za mtoto. Swali liliwataka wanafunzi kuthibitisha kuwa kitendo kinachoonekana katika picha ya mtoto mwenye nyundo mkononi kuwa ni ukiukwaji wa haki za mtoto. Wanafunzi waliondika majibu sahihi katika swali hili walikuwa ni wale ambao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki za mtoto. Wanafunzi hawa waliandika majibu sahihi kama: *kwa sababu ni kazi ngumu kwa mtoto kufanya* na *mtoto anapaswa kuwa shuleni.* Majibu haya yanathibitisha kuwa wanafunzi walikuwa na uelewa wa kutosha kwamba, mtoto ni mwanadamu asiye na ukomavu na anahitaji ushauri-nasihi na mwongozo, upendo na matunzo kwa ajili ya ukuaji mzuri. Kwahiyo, kumuhusisha mtoto katika kazi ngumu za kutengeneza kokoto kwa kugonga gonga mawe ni kuhatarisha afya yake au ukuaji wake kiakili na kimwili. Pia, kuwabakiza watoto nyumbani bila kuwapeleka shule ni ukiukwaji wa haki za watoto kwasababu inawanyima haki ya kupata elimu. Ukiukwaji mwingine wa haki za watoto ni kuwanyima haki ya kustarehe au kupumzika, ajira kwa watoto, ndoa za utotoni, adhabu kali na udhalilishaji. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5.


**Maswali**

(a) Taja matendo mawili yanayoonekana katika picha.

(i) Watoto wanaenda Shule

(ii) Mtotoanaponda mawe ya kokoto

(b) Ni wajibu gani ambao haujatimizwa na wazazi wa baadhi ya watoto wanaoonekana katika picha? Kupeleka watoto Shuleni

(c) Mara unapoona haki za watoto zinakiukwa unatakiwa kufanya nini?

Kutoa taarifa kwa serikali au vyombo vya habari


(d) Kwanini kitendo kinachoonekana katika picha ya mtoto mwenye nyundo mkononi ni cha ukiukwaji wa haki za watoto?

Mtoto anayeonekana katika namba (ii) anatakiwa kupelekwa Shule ili kupata maarifa

Kielelezo 5.1**:** *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 5*

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kutafsiri kitendo cha mtoto kushika nyundo ni wale ambao hawakuwa na ujuzi wa kuchunguza picha na kisha kujibu maswali. Wanafunzi hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kusimamia haki na hivyo waliandika majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya majibu yaliyoandikwa na wanafunzi hawa yalikuwa: *kwa sababu anahitaji pesa kwa ajili ya chakula au mahitaji ya msingi* na *kwa sababu msichana alihitaji pesa mawe.* Wanafunzi walipaswa kuelewa kuwa wazazi au walezi wanawajibika kuwapatia watoto mahitaji ya msingi na huduma kama chakula, malazi, mavazi, huduma za afya na elimu. Kitendo cha kushindwa kutimiza majukumu haya kinawafanya watoto waende mitaani kutafuta riziki na hivyo kusababisha ajira za utotoni. Miongoni mwa wanafunzi hawa yupo aliyeandika: *kwa sababu hakutimiza majukumu yake* na *kwa sababu ni mtoto wa mtaani*. Mwanafunzi huyu alipaswa kufahamu kuwa kanuni ya utu wa binadamu inasisitiza kuwa kila binadamu anastahili kuheshimiwa bila kujali rangi, hali yake ya kijamii, kiuchumi, mfungamano wake na mengine yanayofanana na hayo. Mtoto anastahili kupewa haki zake bila kujali kama anawajibika au hawajibiki: awe ni mtoto wa mitaani au hapana.

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwepo kwa wanafunzi ambao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi. Baadhi ya wanafunzi walitaja majibu ambayo yalihusiana na sababu za matendo ya unyanyasaji wa watoto kama vile: *kwasababu walikuwa hawapendwi na wazazi, unywaji pombe uliokithiri* na *kuendelea kuvuta kwa unyanyasaji kila siku.* Vivyo hivyo, wanafunzi wengine walitaja majibu yanayohusiana na haki na wajibu wawatoto. Baadhi ya majibu hayo yalikuwa: *lazima apate haki yake, ni haki yetu, pata elimu, ni kwenda shule, heshimu watu wengine, watu wengine wanakwenda shule* na *mwamini mtoto*, *hana haki yoyote ya kulindwa* na *ile ya kisasa ni simu.* Mwisho kabisa, uchambuzi ulibaini baadhi ya wanafunzi kuandika herufi na wengine kutoandika jibu lolote, ingawaje swali lilikuwa ni lazima kufanywa. Wanafunzi waliandika herufi kama vile A, B, C na D. Aidha, wanafunzi wengine walikariri vifungu vya maneno kutoka katika swali la 6 na kuvitaja kama jibu la swali. Kwa ujumla, hii inaweza kuwa imesababishwa na wanafunzi hao kukosa umahiri wa somo, kuwa na uwezo mdogo wa lugha katika kuandika au kukosa stadi za KKK. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 5.


**Maswali**

(a) Taja matendo mawili yanayoonekana katika picha.

(i) hushimikiano

(ii) mstahimilifu

(b) Ni wajibu gani ambao haujatimizwa na wazazi wa baadhi ya watoto wanaoonekana katika picha? watoto wa tifu.

(c) Mara unapoona haki za watoto zinakiukwa unatakiwa kufanya nini?

kwaandika wa zazi wako

(d) Kwanini kitendo kinachoonekana katika picha ya mtoto mwenye nyundo mkononi ni cha ukiukwaji wa haki za watoto?

hakizo


Kitendo

Kielelezo Na. 5.2: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 5*

## 2.6. Swali la 6: Kudumisha Amani

Swali lilitungwa kutoka kwenye umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* hususani kutoka umahiri mahususi wa *kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii*. Swali hili lilipima ujuzi wa wanafunzi wa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kisha kuandika majibu katika nafasi zilizoachwa wazi katika kipengele (a) hadi (d). Wanafunzi walitakiwa kusoma kifungu cha habari kilichohusu njia za mawasiliano na kisha kujibu maswali kwa kila kipengele.

Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa kama ifuatavyo: asilimia 47.11 walipata ufaulu wa alama 0 hadi 2, asilimia 19.37 walipata alama 8, asilimia 17.42 walipata alama 6, asilimia 16.10 walipata alama 4. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani wanafunzi 841,944 (52.89%) walipata alama kuanzia 04 hadi 08. Wanafunzi wengine 750,044 (47.11%) walifeli kwa kupata alama kuanzia 0 hadi alama 2. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6**.**




**Kielelezo Na. 6**: *Ufaulu wa wanafunzi katika swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kwa kila kipengele katika swali la 6 ulifanyika kama ifuatavyo:

Kifungu cha habari kilisomeka kama ifuatavyo:
Mawasiliano ni jambo la msingi na la lazima katika jamii yoyote. Mathalan, hapo zamani watu walitumia njia za asili kuwasiliana na kupeana habari. Miongoni mwa njia hizo ni baragumu, ngoma, yowe na sauti mbalimbali za wanyama.

Miaka ya hivi karibuni, njia za mawasiliano zimebadilika sana ambapo njia za kielektroniki hutumika kurahisisha mawasiliano baina ya watu. Miongoni mwa njia hizo za kisasa ni simu, runinga, barua pepe, magazeti na mitandao ya kijamii. Njia hizi za kisasa za mawasiliano ni sehemu ya utandawazi na zimeenea maeneo mengi duniani.

Utandawazi husaidia masuala ya biashara, elimu, michezo na hata siasa. Matumizi mazuri ya utandawazi huleta maendeleo

kwa jamii. Matumizi mabaya ya utandawazi huweza kusababisha kupotea kwa maadili, kushuka kwa kiwango cha elimu na hata yaweza kuwa chanzo cha kutoelewana kati yetu. Kwa hiyo, tunapaswa kutumia utandawazi vizuri kwa maendeleo ya jamii yetu.

Maswali
(a) Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma, taja njia mbili za kisasa za mawasiliano.
(i) ____________________________________________

(ii)____________________________________________

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kutambua njia za kisasa za mawasiliano kwa kuzingatia kifungu cha habari walicho kisoma. Swali liliwataka wanafunzi kutaja njia mbili za kisasa za mawasiliano.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umebaini kuwa wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kusoma kwa makini kifungu cha habari waliweza kuzitaja kwa usahihi njia mbili za mawasiliano ya kisasa. Baadhi ya majibu waliyoyataja wanafunzi yalikuwa: *barua pepe, simu, magazeti, runinga* na *mitandao ya kijamii.* Wanafunzi hawa

walielewa kuwa mawasiliano maana yake ni kusambaza taarifa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa kutumia chombo ambacho kinasambaza taarifa kwa mlengwa katika muda uliopangwa. Vilevile walielewa kuwa mawasiliano ni muhimu kwa jamii yoyote kwani husaidia kukuza ushirikiano, kufanya maamuzi, kuleta ufanisi katika utawala na utendaji kazi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi ambao hawakuwa na ujuzi wa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kisha kuandika majibu walitaja majibu yasiyosahihi. Baadhi ya wanafunzi walishindwa kutofautisha njia za kisasa na njia za zamani za mawasiliano na kutaja majibu kama vile: *ngoma, baragumu* na *kupiga kelele*. Wanafunzi wengine walihusianisha majibu yao na faida za utandawazi kwa kutaja hoja kama vile: *utandawazi unasaidia katika elimu ya biashara, mawasiliano ni muhimu na msingi kwenye kila jamii* na *kupitisha habari*. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa mmoja wa wanafunzi aliandika aina za mawasiliano badala ya njia za kisasa za mawasiliano na hivyo kutaja: *mawasiliano ya mdomo* na *mawasiliano ya ishara*. Mwanafunzi huyu alipaswa kufahamu kuwa mawasiliano ya mdomo hutumia vyote: kuongea na kuandika wakati mawasiliano ya ishara ni njia ambayo binadamu huitumia kueleza hisia, mahitaji, kusudio, wazo au mtazamo bila kutumia lugha ya kuongea bali huhusisha matumizi ya ishara, lugha ya uso na lugha ya mwili.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umebainisha kuwepo kwa kundi la wanafunzi ambao hawakuwa na ujuzi kuhusu ufahamu na hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi. Wanafunzi hawa waliandika majibu ambayo hayakuwa na uhusiano na kifungu cha habari walichotakiwa kusoma. Mfano, walitaja majibu yasiyo sahihi kama vile: *ni sehemu ya utandawazi* na *yanapatika kila kona ya dunia*, *mawasiliano* na *utandawazi*, *iliyopita, nzuri, hawajali wengine na si majukumu yake, kwanini utandawazi* na *wanyama*.

(b) Kwanini utandawazi ni muhimu katika jamii? _______________

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kutathmini umuhimu wa utandawazi katika jamii. Swali liliwataka wanafunzi kueleza umuhimu wa utandawazi katika jamii.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwa wanafunzi ambao walieleza majibu sahihi ya umuhimu wa utandawazi katika jamii waliandika faida za utandawazi kama vile: *inasaidia kwenye biashara, michezo na siasa* na *inaleta maendeleo katika jamii, uchumi na biashara huria ambayo imewezesha bidhaa na huduma kuvuka mipaka kwa masharti nafuu hivyo kuongeza bidhaa na huduma.* Pia, wanafunzi waliandika faida zaidi za utandawazi katika jamii kwa kutaja hoja kama: *ongezeko la bidhaa na huduma, ongezeko la soko la ajira, kuboreshwa kwa teknolojia ya ndani, ongezeko la uwekezaji wa ndani na nje, punguzo la bei ya bidhaa kwa kwa sababu ya ushindani wa kiutandawazi*. Majibu haya yalionesha kuwa wanafunzi walikuwa na ujuzi wa kutosha wa kusoma kifungu cha habari na kisha kuandika majibu. Wanafunzi hawa walielewa kuwa utandawazi ni hali ya kukua kwa muingiliano wa watu, tamaduni, siasa na uchumi ulimwenguni uliosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia hasa teknolojia ya habari na mawasiliano. Utandawazi umeimarisha ushirikiano miongoni mwa nchi mbalimbali duniani kupitia sera ya utawala wa ulimwengu. Baadhi ya vyombo vya serikali vya ulimwengu vya kushughulika na hizo changamoto ni kama vile: Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa, Taasisi ya Biashara ya dunia, Taasisi ya fedha na Mahakama ya Kimataifa ya Haki. Changamoto ya utandawazi ni kukosekana kwa ulinzi, ukiukwaji wa haki za binadamu, umasikini, magojwa na uhalifu wa kimataifa.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umeonesha kuwepo kwa wanafunzi ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa kusoma kifungu cha habari kwa makini na kisha kuandika majibu. Wanafunzi hawa walishindwa kuandika majibu sahihi na hivyo kuandika hoja zisizohusiana na kifungu cha habari walichopewa. Baadhi ya majibu waliyoyaandika yalikuwa; *kwa sababu ya utandawazi na upo kwenye nchi nyingi* na *sehemu mbalimbali ulimwenguni, vizuri utandawazi kupata habari*, *kwa sababu inafanya mawasiliano na kuharakisha vitu mbalimbali.* Majibu

mengine ya wanafunzi yalikuwa; *inaweza kusababisha kutokuelewana miongoni mwetu, magazeti na mitandao ya kijamii kwa watu, watu walitumia njia za kiasili kwa mawasiliano na kusambaza habari, wanyama, mitandao jamii, sehemu za ulimwengu, kukosekana kwa maadili* na *karibuni njia mabadiliko makubwa*.

(b) Watu waliwasilianaje hapo zamani? ____________________.

Swali hili lilipima uwezo wa wanafunzi kubaini njia zilizotumiwa na jamii hapo zamani kuwasiliana. Wanafunzi waliosoma na kuelewa vizuri kifungu cha habari na waliweza kubaini majibu sahihi kwa kutaja njia za kiasili zilizotumika kuwasiliana. Baadhi ya njia hizo zilikuwa: *pembe, ngoma, kupiga kelele kwa sauti* na *sauti mbali mbali za wanyama.* Wanafunzi hawa walielewa kuwa pembe ni chombo cha sauti ambacho kimetengenezwa au ni umbo la pembe ya mnyama ambayo inapulizwa kwenye tundu ili kutoa ishara fulani ambayo inawasilisha taarifa maalum inayofika mbali. Hiki kifaa kilitumiwa kiasili kati ya jamii za wafugaji, wakulima na wawindaji kwa ajili ya kuwatisha na kuwahadaa wapiganaji wa makabila mengine pinzani, kuwatahadharisha watu kuanza kwa vita au dalili ya kuvamiwa na adui. Pia, ilitumika kutaarifu kuanza kwa vita, kutangaza kurudi kwa mashujaa kutoka vitani. Mahali pengine, wakulima hutumia kufukuza wanyama hatari. Kwa upande wa ngoma wanafunzi walifahamu kuwa zilikuwa zikichezwa kwa kupiga kwa kijiti kimoja au viwili au kwa mkono kutegemeana na aina ya sauti inayokusudiwa. Walijua pia kuwa kila mdundo wa ngoma uliwasilisha ujumbe tofauti tofauti. Kwa mfano, kulikuwa na ujumbe mbalimbali ulioashiria sherehe, misiba, mikutano, matangazo ya vita, kuashiria ujio wa wageni na uvamizi. Mdundo wa kwanza uliposikika tu, wapiga ngoma wengine waliupokea kwa mapigo mengine ya ngoma na kusambaza sehemu zingine ili usambae mbali zaidi. Vilevile, sauti za kelele zilifanyika milimani kwa ajili ya kuongeza mwangwi uende mbali. Aina mbalimbali za kelele zilimaanisha ujumbe tofauti tofauti kwa mfano kupiga yowe kulimaanisha habari mbaya wakati kupiga vigelegele kuliashiria furaha. Aidha, njia nyingine za mawasiliano zilihusisha: kukimbiza ujumbe ambao ulikimbizwa na watu walioaminika kuwasilisha


ujumbe wa haraka zaidi ulioandikwa kwa njia ya picha au alama. Hivi vilirekodiwa kwenye karatasi maalum, mawe na ngozi za wanyama. Nyingine ilikuwa ni ishara ya moto. Moto huu ulikuwa unawashwa kwenye milima au miinuko ambapo kila mmoja anaweza kuona kutoka mbali na uliwekwa kwa namna ambayo adui asingeweza kutafsiri ujumbe wake kirahisi. Ilikuwa kwa ajili ya kutoa taarifa ya uvamizi wa maadui au kuwasilisha ujumbe muhimu.

Mwisho kabisa, uchambuzi umeonesha kuwepo kwa wanafunzi ambao walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Wanafunzi hawa walinakiri maswali kutoka katika vipengele vya maswali mengine. Kwa mfano, mmoja wa wanafunzi aliandika majibu ya swali la kipengele (a) kilichouliza umuhimu wa utandawazi katika jamii. Mwanafunzi huyu alitaja: *kupata taarifa na kusaidia elimu*, *maendeleo, matumizi ya utandawazi kwa maendeleo jamii* na *kusambaza habari*. Vilevile, mwanafunzi mwingine alitaja majibu ya swali la kipengele (b) ambalo lilimtaka mwanafunzi kutaja njia mbili za kisasa za mawasiliano badala ya njia zilizotumiwa na jamii hapo zamani kuwasiliana. Mwanafunzi alitaja: *mawasiliano kwenye hii simu*, *runinga, barua pepe* na *magazeti, kwa kutumia simu, runinga redio* na *simu-janja ni sehemu ya mawasiliano.*

(d) Kwanini tunapaswa kutumia utandawazi vizuri? _____________

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kuchambua athari za utandawazi kwa kurejea katika kifungu cha habari walichokisoma. Swali liliwataka wanafunzi kuelezea sababu zinazoifanya jamii kutumia utandawazi vizuri. Wanafunzi waliokuwa na ujuzi wa kutosha kusoma kwa umakini kifungu cha habari na kisha kuandika majibu waliweza kubaini jibu sahihi *inaleta maendeleo katika jamii*. Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utandawazi, walielewa kuwa unaweza kusababisha madhara chanya na hasi katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Walijua kuwa matumizi mazuri ya utandawazi yanaweza kupelekea ongezeko la upatikanaji wa bidhaa na huduma kwenye soko, upanuzi wa biashara ya ndani na nje ya nchi kutokana na kupungua kwa vizuizi, kusambaa kwa lugha za kimataifa kama: Kichina, Kiingereza, Kiarabu na Kifaransa ambazo

zimewezesha na kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii mbalimbali duniani. Faida nyingine za utandawazi ni kukua kwa uchumi wa nchi kutokana na uwekezaji kutoka mataifa ya nje na mikopo ambayo imewezesha serikali kujenga miundombinu ya barabara, reli, madaraja, hospitali, shule na miradi mingine ya kimkakati. Kwa upande mwingine, wanafunzi walielewa hasara za utandawazi katika jamii ambazo ni kudhoofisha viwanda vya ndani kufuatia uingizwaji mkubwa wa bidhaa kutoka nje zinazouzwa kwa bei nafuu na utegemezi wa kiteknolojia. Aidha, wanafunzi walielewa kuwa athari nyingine ni kama vile: kuzorota kwa usalama na kuongezeka kwa uhalifu wa kimataifa unaosababishwa na kuzagaa kwa silaha haramu, madawa ya kulevya na ugaidi. Utandawazi pia unaweza kudhoofisha utamaduni wa jamii kwani muingiliano na tamaduni nyingine za nje hupelekea kuiga tamaduni zisizofaa katika jamii zetu. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi kwa swali la 6.



**Maswali**

(a) Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma, taja njia mbili za kisasa za mawasiliano.

(i) simu runinga

(ii) barua pepe magazeti na mitandao ya kijamii

(b) Kwanini utandawazi ni muhimu katika jamii? Matumizi mazuri ya utandawazi uleta maendeleo kwa jamii


(c) Watu waliwasilianaje hapo zamani? waliwasiliana na baragumu ngoma yowe na sauti mbalimbali za wanyama

(d) Kwanini tunapaswa kutumia utandawazi vizuri? tunapaswa kutumia utandawazi vizuri kwa maendeleo ya jamii yetu.

Kielelezo Na. 6.1: *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6*

Uchambuzi zaidi wa majibu umebainisha uwepo wa wanafunzi ambao waliandika majibu ambayo hayakuwa na uhusiano na mahitaji ya swali. Hii inaweza kuwa ilisababishwa na wanafunzi kukosa uwezo wa kusoma kwa makini kifungu cha habari. Baadhi ya majibu waliyoandika wanafunzi hawa yalikuwa: *kwa sababu haileti mmomonyoko mbaya wa maadili katika jamii yetu*, *magazeti*

*na mitandao ya kijamii kwenye jamii yetu*, *inaweza kusababisha kupotea kwa maadili na kupungua ubora wa elimu*. Majibu mengine ya wanafunzi yalikuwa: *biashara* na *elimu*, *utandawazi wa njia nzuri umepungua* na *barua pepe* na *runinga*. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6.


**Maswali**

(a) Kutokana na kifungu cha habari ulichosoma, taja njia mbili za kisasa za mawasiliano.

(i) Kifungu

(ii) Kwanini

(b) Kwanini utandawazi ni muhimu katika jamii? zamani utandawazi

(c) Watu waliwasilianaje hapo zamani? Utandawazi kutumia

(d) Kwanini tunapaswa kutumia utandawazi vizuri? kutumia kwanini

Kielelezo Na. 6.2: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mwanafunzi katika swali la 6*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Uchambuzi wa umahiri katika maswali ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Uraia na Maadili unaonesha kuwa kati ya mahiri 6 zilizopimwa ni mahiri 1 pekee ambayo imekuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Umahiri huo ni *Kuwa Mwajibikaji* ambao uliulizwa katika swali la 1 (68.25%). Aidha kwa kulinganisha, umahiri wa *Kuheshimu Jamii* katika swali la 2 (61.68%), *Kuithamini Jamii* katika swali la 4 (56.60%), *Kuwa Mstahimilivu* katika swali la 3 (55.27%) na *Kudumisha Amani* katika swali la 6 (52.89%) ulikuwa na ufaulu wa wastani. Kwa upande mwingine, umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* katika swali la 5 (31.33%) umekuwa na ufaulu hafifu.

Aidha, ulinganifu wa ufaulu wa umahiri kati ya upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne kwa mwaka 2021 na 2022 unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu cha umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* umeongezeka

kutoka ufaulu wa wastani (51.4%) katika mwaka 2021 hadi ufaulu mzuri (68.25%) katika mwaka 2022. Ufaulu katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii* umeendelea kuwa wa wastani (54.8%) katika mwaka 2021 na (61.68%) katika mwaka 2022. Ufaulu katika mahiri nyingine ni kama ifuatavyo: *Kuwa Mwadilifu* ufaulu umepungua kutoka kuwa ufaulu mzuri (76.9%) katika mwaka 2021 hadi ufaulu dhaifu (31.33%) katika mwaka 2022. Vivyo hivyo, ufaulu katika umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* umepungua kutoka kuwa mzuri (67.3%) katika mwaka 2021 hadi ufaulu wa wastani (55.27%) katika mwaka wa 2022. Katika umahiri wa *Kuheshimu Jamii,* ufaulu umeendelea kuwa wa wastani (54.8%) katika mwaka 2021 na 61.68% katika mwaka 2022. Mwisho, katika umahiri wa *kudumisha Amani,* ufaulu umeongezeka kuwa wa wastani kutoka dhaifu (17%) 2021 hadi wastani (52.89%) katika mwaka 2022.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne katika somo la Uraia na Maadili umeonesha kuwa kwa ujumla wanafunzi wamefaulu kwa kiwango cha wastani. Wanafunzi waliopata Daraja A hadi D walikuwa asilimia 84.85 ilhali wachache ambao ni asilimia 15.15 wamepata kiwango hafifu cha ufaulu wa Daraja E. Wanafunzi waliofanya vizuri katika upimaji huu walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mahiri zilizopimwa. Aidha, wanafunzi hawa waliweza kubaini matakwa ya maswali na walionesha kuwa na stadi ya Kusoma na Kuandika.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi umebaini changamoto mbalimbali walizokuwa nazo wanafunzi na hivyo kuwa na ufaulu hafifu. Baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mahiri zilizopimwa, kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa stadi za kusoma na kuandika na hivyo kushindwa kuandika majibu yanayoeleweka. Vilevile, wanafunzi walionesha ukosefu wa umahiri katika maswali ya stadi za kuangalia picha kwa umakini na kisha kujibu maswali, na kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali katika swali la 5 na 6 mtawalia.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Uraia na Maadili, Baraza la Mitihani linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wa somo kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi umahiri unaokusudiwa. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na:

(i) Maigizo dhima, kujifunza kwa kuuliza na ujifunzaji wa ushirikiano; mbinu ambazo hujumuisha matendo kama: fikiri na kushirikiana wawili, majadiliano katika makundi madogo au wawili. Hii itasaidia kuboresha Maarifa ya kijamii na uwezo wa mwanafunzi kufikiri vizuri.

(ii) Matumizi ya michezo mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hii hugeuza mapenzi ya mtoto kupenda michezo kuwa mapenzi ya kupenda kusoma. Hivyo, humfanya mtoto kutilia mkazo shughuli za darasani na hatimaye kupata ujuzi uliotarajiwa.

(iii) Kutumia mbinu ya kutembelea maeneo mbalimbali ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza mahiri mbalimbali za somo.

(b) Walimu na wazazi kubuni mbinu za kuwawezesha wanafunzi kupenda kujisomea vitabu vya kiada na ziada ili kuimarisha uelewa wa mahiri za somo la Uraia na Maadili.

(c) Walimu kuongeza jitahada za kuchunguza na kung'amua uimara na udhaifu wa kila mwanafunzi na kutafuta namna ya kumsaidia.

(d) Wanafunzi wapatiwe shughuli nyingi za upimaji wa mahiri darasani kama vile mazoezi, majaribio na mitihani ili kuboresha uwezo wao wa kujibu maswali. Shughuli hizo zilenge kupima stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na ufahamu.

*Kiambatisho*

**Ulinganifu wa ufaulu kwa wanafunzi katika kila umahiri kwa mwaka 2021 na 2022**

| | | UPIMAJI 2021 | | | UPIMAJI 2022 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu wa kila swali | W a | Ma oni | Ufaulu wa kila swali | W a | Ma oni |

| | Umahiri | Namba ya swali | % ya ufaulu | | | Namba ya swali | % ya ufaulu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuwa Mwajibikaji | 6 | 51.4 | 51.4 | Wastani | 1 | 68.25 | 68.25 | Vizuri |
| 2 | Kuheshimu Jamii | 2 | 54.8 | 54.8 | Wastani | 2 | 61.68 | 61.68 | Wastani |
| 3 | Kuithamini Jamii | 3 | 66.8 | 66.8 | Vizuri | 4 | 56.60 | 56.60 | Wastani |
| 4 | Kuwa Mstahimilivu | 5 | 67.3 | 67.3 | Vizuri | 3 | 55.27 | 55.27 | Wastani |
| 5 | Kudumisha Amani | 4 | 17 | 17 | Hafifu | 6 | 52.89 | 52.89 | Wastani |
| 6 | Kuwa Mwadilifu | 1 | 76.9 | 76.9 | Vizuri | 5 | 31.33 | 31.33 | Hafifu |